



Upimaji wa COVID-19

Je, ninapaswa kupata kipimo cha COVID-19 lini?

- Una dalili za COVID-19.
- Uko katika [hatari kubwa ya ugonjwa mbaya](#) na hivi karibuni umekuwa na mfiduo wa hivi karibuni na mtu aliye na COVID-19.
- Wewe ni mtu wa kaya yake au umekuwa na mfiduo wa hatari kubwa au kadirifu kwa mtu aliye na COVID-19.



Nani aliye ana hatari kubwa ya ugonjwa mbaya?

- Watu wa umri wa miaka 60 na zaidi
- Wanawake wajaawazito
- Watu wa Asili, wa Visiwa vya Torres Strait na vya Pasifika (kuanzia miaka 35 na zaidi)
- Watu wenye fetma, ugonjwa wa kisukari, ugonjwa mkubwa wa moyo na mishipa, ugonjwa wa mapafu ya muda mrefu (*ukiwemo pumu kali inayotakiwa kulazwa hospitali katika miezi 12 iliyopita*), ugonjwa mbaya sugu wa ini au figo, saratani hai au ambaye ana kingamwili dhaifu
- Watu wengine wenye ulemavu wakiwemo wale wenye ulemavu unaoathiri mapafu yao, mioyo yao, au mfumo wao wa kinga
- Wakazi wa vituo vya huduma za wazee na walemavu
- Watu wenye umri wa miaka 18 na zaidi ambao hawajachanjwa

Je, ni kipimo gani cha COVID-19 ninachopaswa kupata?


Kuna **vipimo viwili tofauti** unaweza kupata ili kuangalia kama unaugua COVID-19. **Kipimo cha haraka cha antijeni** (RAT) ambacho unaweza kufanya wewe mwenyewe na **kipimo cha PCR** (usufi wa pua na koo) ambacho kinafanywa katika kliniki cha kipimo.

- **Ikiwa uko katika hatari kubwa wa ugonjwa mbaya** unapaswa kupata **kipimo cha PCR**. Ikiwa huwezi kupata jibu la kipimo cha PCR haraka, fanya kipimo cha haraka cha antijeni (ikiwa unacho) wakati unaposubiri jibu la kipimo cha PCR.
- Ikiwa **huna** hatari kubwa ya ugonjwa mbaya, fanya kipimo cha haraka cha antijeni isipokuwa daktari wako atakuambia ufanye kipimo cha PCR.



Je, nitafanya nini nikipimwa kuwa na COVID-19?

- Ikiwa umepata matokeo **chanya** ya kipimo cha **PCR**, hata kama huna dalili, unaugua COVID-19. Lazima ufuate ushauri kwa watu [wanaopata jibu chanya ya kipimo cha COVID-19 na kudhibitisha COVID-19 kwa usalama nyumbani](#).
- Ikiwa umepata kipimo chanya cha haraka cha antijeni [andikisha jibu lile na Service NSW](#) na fuata ushauri kwa watu [wanaopata jibu chanya la kipimo cha COVID-19 na kudhibitisha COVID-19 kwa usalama nyumbani](#).



Ikiwa una shida yoyote ya kiafya na unahitaji usaidizi wa lugha, piga simu kwenye **TIS 131 450** na omba kwa Health Direct kwenye nambari ya simu kwenye **1800 022 222**.